



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UCHAGUZI MDOGO WA MAJIMBO YA
KONDE MKOA WA KASKAZINI PEMBA NA USHETU MKOANI SHINYANGA.**

Dodoma, 27 Agosti, 2021

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepokea barua kutoka kwa Mhe. Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenye Kumb. Na. CEA.137/400/02/111 ya tarehe 16 Agosti 2021, akiitaarifu kuhusu kuwepo kwa nafasi wazi ya Ubunge katika Jimbo la Ushetu Mkoani Shinyanga. Nafasi hiyo inatokana na kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, Mheshimiwa **Elias John Kwandikwa** wa Chama Cha Mapinduzi (CCM). Taarifa hiyo ya Mheshimiwa Spika ni kwa mujibu wa kifungu cha 37(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343.

Aidha, itakumbukwa kuwa Tume, tarehe 2 Agosti, 2021 ilitoa taarifa kwa umma kuhusu kuwepo wazi kwa Jimbo la Konde lilipo katika Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba kutokana na mbunge mteule wa jimbo hilo **Ndugu Sheha Mpemba Faki** kujiuzulu.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa Tume ilipokea barua yenye Kumb. Na. CMM/T.40/Vol.I/72 ya tarehe 2 Agosti, 2021 kutoka kwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ikitoa taarifa kuwa Mbunge Mteule wa Jimbo la Konde, ameandika barua, kueleza kwamba hakuwa tayari kuwakilisha wananchi wa Jimbo la Konde kutokana na changamoto za kifamilia. Kutokana na hatua hiyo, Tume ililitangaza jimbo hilo kuwa

wazi kwa kuwa Mbunge huyo Mteule alikuwa bado hajatangazwa katika Gazeti la Serikali kwa mujibu wa kifungu cha 81(c) (iii) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343.

Awali mnamo tarehe 18 Julai, 2021 Tume iliendesha Uchaguzi mdogo katika Jimbo la Konde kujaza nafasi iliyoachwa wazi kutokana na kifo cha aliyekuwa Mbunge wa jimbo hilo Mheshimiwa **Khatibu Saidi Haji** kupitia chama cha **Alliance for Change and Transparency (ACT -WAZALENDO)**

Katika kujaza nafasi hizo, Tume imepanga ratiba ya Uchaguzi mdogo wa Jimbo la Konde, Mkoa wa Kaskazini Pemba na Jimbo la Ushetu, Mkoa wa Shinyanga kama ifuatavyo:-

Na.	TUKIO	TAREHE
1.	Wagombea kuchukua fomu za uteuzi	13 - 19 Septemba, 2021
2.	Uteuzi wa wagombea	19 Septemba, 2021
3.	Kampeni za Uchaguzi	20 Septemba - 08 Oktoba 2021
4.	Siku ya kupiga kura	09 Oktoba 2021

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inavikumbusha vyama vya siasa na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi, taratibu, miongozo na maelekezo yatakayotolewa na Tume katika kipindi cha Uchaguzi mdogo.


Dkt. Wilson Mahera Charles

Mkurugenzi wa Uchaguzi

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI